

Maswali

1. Mbona Mungu alichagua nabii mwingine kusaidia Eliya?
2. Nabii mpya alikuwa nani?
3. Pahali pawili penye Eliya alienda kusema kwaheri kwa manabii ni wapi?
4. Nani alitaka kwenda naye?
5. Eliya na Elisha walivuka mto wa Yordani namna gani?
6. Elisha aliuliza Eliya amfanyie nini?
7. Elisha alitakiwa afanye nini ili apate nguvu za Mungu?
8. Elisha aliona nini?
9. Eliya alichuguliwa namna gani?
10. Elisha akirudi, alivuka Mto wa Yordani namna gani?

Majibu

1. Eliya alikuwa anakua mzee na kulitakiwa kuwe na nabii mwingine wa kuendesha kazi ya Mungu.
2. Elisha ndiye alikuwa nabii mpya.
3. Eliya alienda Betheli na Yeriko kupeana manabii kwaheri.
4. Elisha alitaka kwenda naye.
5. Eliya alipiga mto kwa joho lake na maji yakagawanyika.
6. Elisha aliuliza apewe maradufu nguvu za Mungu.
7. Ililazimu Elisha aone Eliya akichukuliwa.
8. Aliona farasi na magari ya moto.
9. Eliya alichukuliwa kwa kibunga cha nguvu.
10. Eliya alitupa joho lake. Elisha alichukua na kulipigia maji. Mto uligawanyika na akavuka.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



32 Eliya na Elisha

Marejeo

2 Wafalme 2: 1 – 15

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anachagua watu waaminifu kuendelesha kazi yake.

Maneno maalum

- 32.1 Eliya + mzee +Mungu alichagua + kijana + Elisha + saidia
- 32.2 Mungu + Eliya + sema kwaheri + Elisha baki? + hapana + Betheli + Eliya anaenda + sema kwaheri + Elisha baki + hapana + Yeriko + Eliya anaenda + sema kwaheri
- 32.3 Eliya + Elisha + Mto wa Yordani + piga na joho + mto ukagawanyika + vuka n'gambo
- 32.4 Eliya + Elisha + unataka nini? + nguvu maradufu + ukiona Eliya akichukuliwa + farasi na gari ya moto + kibunga + Eliya + mpaka angani
- 32.5 Eliya + angusha joho + Elisha + piga maji + gawanyika + vuka n'gambo + Elisha kiongozi mpya

32.1 Eliya alikuwa anaendelea kuwa mzee kwa hivyo Mungu akachagua Elisha kiongozi kijana asaidie kwa kazi ya Mungu. Eliya alipata Elisha akilima na jozi kumi na mbili za n'gombe. Eliya alimuuliza Elisha aende naye amsaidia kwa kazi ya Mungu.

Elisha alimwambia Eliya, "Tafadhalii niaje niende niwape baba na mama yangu kwaheri halafu nikuje nikusaidie." Elisha alienda akaita jamii yake kwa karamu. Ilikuwa karamu ya kwaheri. Baada ya karamu Elisha alienda na Eliya kumsaidia kazi ya Mungu. Eliya alifundisha Elisha vile atafanya kazi ya Mungu.

32.2 Ilifika wakati fulani baadaye, Eliya alikuwa amemaliza kazi yake kama nabii. Mungu alikuwa amemchagua Elisha kuwa nabii baada ya Eliya na afanye kazi ya Mungu yenye Eliya alikuwa akifanya. Mungu aliambia Eliya aende ambie manabii vijana kwaheri. Eliya aliambia Elisha, "Utapenda kukaa hapa kwa sababu Mungu amenituma Betheli?" Lakini Elisha alijibu, "Sitakuacha." Kwa hivyo walienda wote Betheli.

Kule Betheli, baadha ya manabii vijana walikuja kuambia Elisha, "Unajua kwamba Bwana atamchukua Eliya leo?" Elisha alijibu, "Ndiyo ninajua." Eliya aliwapa manabii wa Betheli kwaheri. Tena Eliya akaambia Elisha, "Utapenda kukaa hapa kwa sababu Mungu amenituma Yeriko?" Lakini Elisha alijibu, "Sitakuacha." Kwa hivyo walienda wote Yeriko.

Kule Yeriko, baadhi ya manabii vijana walikuja kuambia Elisha kwamba, "Unajua kwamba Bwana atachukua Eliya leo?" Elisha alijibu, "Ndiyo ninajua." Eliya aliwapa manabii wa Yeriko kwaheri.

32.3 Wakati manabii vijana walikuwa wakiangalia, Eliya na Elisha walitembea wakaenda kwa Mto wa Yordani. Watavuka namna gani? Eliya alichukuwa joho lake akalikunja na kupiga kwa maji. Aliomba Mungu asaidie. Halafu mto ukagawanyika ili hawa watu wawili watembee kwa nchi kavu.

32.4 Eliya aliuliza Elisha kama anakitu chenye anataka amfanyie kabla hajachukuliwa. Elisha alijua ana kazi nyingi ya kufanya kama nabii wakati Eliya hatakuweko tena kumsaidia. Eliya alikuwa na nguvu za Mungu iliyokuwa ikimsaidia kwa kazi zake. Elisha alijua anatakiwa hii nguvu za Mungu hata zaidi ya yenye Eliya alikuwa nayo. Kwa hivyo aliambia Eliya, "Tafathali, nisaidie niwe na nguvu za Mungu maradufu zako. Eliya alimwambia kwamba hiyo ilikuwa vigumu kwa sababu huo uwezo unapatikana kwa Mungu. Lakini Eliya akamwambia eti akimwona akichukuliwa, atapata hizo nguvu za Mungu.

Walipokuwa wakizungumza na kutembea, farasi ya moto na gari la moto vilikuja katikati yao. Hiyo farasi na gari vilin'gaa kwa mwangaza mwingi kama vimeundwa kutoka kwa moto.

Kibunga cha nguvu kilivuma, kikachukua Eliya juu angani. Elisha hakuona Eliya wala farasi na gari tena. Lakini aliona kila kitu kikifanyika, kwa hivyo alijua kwamba atakuwa na nguvu za Mungu kumsaidia.

32.5 Eliya aliangusha joho lake chini na Elisha akaichukuwa na akarudi kwa mto. Ataweza kuvuka vile Eliya alifanya? Elisha alipiga mto na joho lenye Eliya alikuwa ameangusha na akaomba vile Eliya alikuwa amefanya. Maji yaligawanyika na Elisha akavuka kwa nchi kavu. Wale manabii vijana walikuwa wakiangalia na wakasema, "Elisha alikuwa na nguvu za Mungu vile Eliya alikuwa." Walienda kukutana naye kwa sababu yeye alikuwa sasa ni kiongozi wao. Mungu alikuwa na Elisha na akafanya miujiza mingi.

